



Mpando wa karibu...

Hukuwezesha kupata majani mengi and ya hali ya juu kutoka kwa shamba lile lile

... itatoa nafasi kwa nyasi ya 'Napier' kukua na kutumiwa badaaye

... vile vile majani ya mahindi itapatikana wakati wa upungufu wa majani mengine ya ng'ombe


.... isitoshe itakuokolea pesa za kununua majani ya ng'ombe

Njia moja ya kuongeza majani ya ng'ombe na maziwa




Kupata majani mengi kutoka kwa mahindi, tumia moja yapo ya njia zifuatazo....

- Panua mashimo ya kupandia mara mbili ya kawaida na upande mbegu 4 – 5 kwa kila shimo.



- Punguza upana katikati ya mashimo na usipande zaidi ya mbegu 4 kwa kila shimo



- Punguza upana katikati ya misitari ya mahindi na usipande zaidi ya mbegu 4 kwa kila shimo



Changanya vizuri samadi na mbolea ya dukani pamoja na mchanga kabla ya kupanda mbegu au panda mbegu mchagani kando kando ya shimo. Hii itahakikisha mbolea haitaanguza mbegu.




Panda maharagwe katikati mwa misitari ya mahindi badala ya kupanda kwa shimo moja na mahindi. Panda maharagwe na mahindi wakati mmoja.



TARATIBU YA KWANZA YA UPANZI

Shimo la kupanda



TARATIBU YA PILI YA UPANZI


Shimo la kupanda



Tawanya mbegu kwa shimo ukitumia moja yapo ya njia zilizo onyeshwa hapo juu




TARATIBU YA TATU YA UPANZI




ama unaweza kupanda kwa mtaro

Compiled by: Bernard Lukuyu and Priscillah W. Ndegwa
Leaflet supported and funded by DIFD through The Small Holder Dairy Project

Kipimo cha kawaida cha mbolea ya dukani ni kifuniko kimoja cha chupa ya 'fanta' ama kijiko cha chai kidogo kimoja kwa kila shimo. Nacho kipimo cha samadi viganja viwili kama vimejaa kwa kila shimo. Ukipanda karibu karibu tumia mara dufu ya vipimo hivi.



Mbolea ya dukani



Samadi



Kupata majani ya ng'ombe kutoka kwa mahindi...

- 1 Ngoa mihindi miembamba, midhaifu na migonjwa wakati unapopalilia
- 2 Punguza mimea ya mihindi kulingana na mahitaji ya majani ya ng'ombe mpaka mumea uchanue
- 3 Baada ya mahindi kuchanua, punguza mimea kwa kung'oa na kulisha ng'ombe hadi ubakishe mimea miwili ikomee.
- 4 Iwapo kuna upungufu wa mvua na mahindi yasizaliwe, lisha mmea wote kwa ng'ombe.



Ukipanda mahindi karibu karibu, huenda ukapata mahindi mengi lakini madogo madogo.

Mazao ya maharagwe hupungua iwapo maharagwe yamepandwa pamoja na mahindi



Mahindi yakipandwa karibu karibu hunipatia ...

- 1 mihindi ya kupunguzwa kwa chakula cha ng'ombe
- 2 Ufefe wa mahindi mbichi kwa chakula cha ng'ombe
- 3 mahindi yaliyo kauka kwa chakula changu
- 4 mahindi mbichi ya kuuza
- 5 Ufefe wa mahindi uliokauka kwa chakula cha ng'ombe
- 6 hutumia mmea wa mahindi kwa chakula cha ng'ombe wakati kuna upungufu wa mvua na mahindi hayakuzaliwa.



PATA ZAIDI KUTOKA KWA MAHINDI

Panda mahindi karibu karibu!